TANGAZO LA SERIKALI NA. 219 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153)*

## SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA KUZUIA NA KUDHIBITI SUMUKUVU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO YA MWAKA 2025

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Kuzuia na Kudhibiti Sumukuvu ya Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Kuzuia na Kudhibiti Sumukuvu ya Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

TS. Na. 269 la 2024

Marekebisho ya kanuni ya 13

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 13 kwa-

(a) kupangilia upya masharti ya kanuni hiyo kuwa kanuni ndogo ya (1);

(b) kuondoa maneno "vifungashio na" yaliyopo katika kanuni ndogo ya (1) iliyopangiliwa upya; na

(c) kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (1) iliyopangiliwa upya kanuni ndogo mpya ifuatayo:

"(2) Mmiliki wa mazao anayesafirisha mazao yake anapaswa kuhakikisha vifungashio na vifaa anavyotumia kusafirisha mazao ni vikavu au visivyoruhusu maji au unyevu na vumbi kuingia ndani ili kuepusha kuvu kuota

kwenye mazao.”.

Marekebisho ya kanuni ya 16

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 16 kwa-

(a) kuongeza maneno “bila kuwa na sababu ya msingi” mwanzoni mwa aya za (a), (b) na (c); na

(b) kufuta neno “hataanika” lililopo mwanzoni mwa aya (d) na badala yake kuweka maneno “ataanika mazao”.

Dodoma,
10 Januri, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*